Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. BDC/S.3/26/VOL.II/42 16/02/2023

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Butiama kwa kuzingatia kibali cha ajira mbadala cha tarehe 19/12/2022 chenye Kumb. Na. FA. 170/377/01" B"/130 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – UTUMISHI. Anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi: -

## DEREVA DARAJA LA II NAFASI (01)

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kuendesha gari la abiria na malori.
ii. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
iii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
iv. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari
vi. la safari.
vii. Kufanya usafi wa gari na
viii. Kufanya kazi nyingine kadili utakavyoelekezwa na msimamizi wako.

### 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

i. Awe Mtanzania mwenye cheti cha kuzaliwa na kitambulisho au namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA).
ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na lessen ya udereva daraja c.
iii. Awe na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitano (5) bila kusababisha ajali.
iv. Awe na cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II au sifa nyingine iliyolingana nayo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
v. Awe na umri wa miaka 18 au Zaidi na asiwe na umri unaozidi miaka 45.
vi. Awe na afya njema, mchapa kazi na mwenye utayari wa kufanya kazi ya udereva katika Halmashauri ya Wilaya ya Butiama.



Scanned with CamScanner

## 2.0 NAMNAYA KUOMBA

a) Testimonials 'Provsional Results", Statement of Results; Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAMBULIKI.**
b) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na kwa lugha ya kishwahili au kiingereza tofauti na hapo maombi hayatapokelewa.
c) Taarifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
d) Waombaji wote waambatishe maelelzo binafsi (detail CV), yenye anuani na namba za simu zinazopaatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.

3. Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikal **TGS 'B'**

## 3.1 MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

Maombi yatapokelewa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) – Butiama, mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 08/03/2023 saa 9.30 Alasiri

Tunawakaribisha wote wenye sifa zilizotajwa hapo juu kuwasilisha maombi yao kwa utaratibu ulioelekezwa. Maombi yote yatumwe kupitia amwani ya:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya wilaya Butiama
S.L.P. 1207,
**BUTIAMA**

**Nakala:** Katibu,
Sekretariet ya ajira,
Jengo la Asha Rose Migiro,
Chuo Kikuu cha Dodoma,
S.L.P 2320,
**DODOMA.**

Tangazo hili linapatikana kwenye mbao za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Butiama pamoja na kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ambayo ni www.butiamadc.go.tz na kwenye tovuti ya sekretarieti ya ajira http/www.ajira.go.tz



MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA BUTIAMA

Scanned with CamScanner